



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UAMUZI WA RUFEEA ZA
WAGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI

Dar es Salaam, 13 Septemba, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha jana tarehe 12 Septemba 2020 imepitia, imechambua na kuzifanyia uamuzi rufaa za wagombea Ubunge na Udiwani zilizowasilishwa na wagombea kupitia kwa Wasimamizi mbalimbali wa Uchaguzi nchi nzima.

Rufaa hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 40(6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kikisomwa pamoja na kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa Ubunge na Udiwani kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Aidha, chini ya kanuni ya 32 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, ikisomwa pamoja na kanuni ya 30 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2020, Tume inaweza kukubali au kukataa rufaa hizo.

Katika kikao hicho, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufaa 50, kati ya hizo rufaa 4 ni za Wagombea Ubunge na 46 ni za Wagombea Udiwani.

Kwa upande wa rufaa za wagombea Ubunge, Tume imekataa rufaa zote nne ambazo ni za wagombea ambao uteuzi wao ulitenguliwa. Kwa hiyo, wagombea hao wanaendelea kutokuwa kwenye orodha ya wagombea. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Jimbo la Babati Mjini.


Aidha, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi rufaa 46 za Madiwani, kama ifuatavyo:-

- i. Imekubali rufaa 25 na kuwarejesha wagombea Udiwani katika orodha ya wagombea Udiwani. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Changaa (Kondoa), Kichonda (Liwale), Kisima (Same Magharibi), Kibada (Kigamboni), Utende (Katavi), Myamba (Same Mashariki), Buswelu (Ilemela), Kiseke (Ilemela), Kimochi (Moshi Vijijini), Kikilo (Kondoa), Bereko (Kondoa), Isanga (Maswa Magharibi), Kirumba (Ilemela), Liwale Mjini (Liwale), Mshewe (Mbeya Vijijini), Nar (Babati Vijijini), Namiungo (Tunduru Kaskazini), Kimbiji (Kigamboni), Chitete (Ileje), Dunda (Bagamoyo), Kimambi (Liwale), Ludewa (Ludewa), Mwabusalu (Kisesa), Konje (Handeni Mjini) na Makurumla (Ubungo)
- ii. Imekataa rufaa 12 za wagombea Udiwani ambao hawakuteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Mwayaya (Buhigwe), Bwakira Chini (Morogoro Kusini), Lalago (Maswa Mashariki), Duga

(Tanga Mjini), Makurumla (Ubungo), Ngoywa (Sikonge), Isyesye (Mbeya Mjini), Iwambi (Mbeya Mjini), Oltrumet (Arumeru Magharibi), Iyunga (Mbeya Mjini), Bumilayanga (Mafinga Mjini) na Kahangara (Magu).

- iii. Imekataa rufaa 9 za kupinga wagombea Udiwani walioteuliwa. Rufaa hizo ni kutoka kwenye Kata za Maendeleo (Mbeya Mjini), Forest (Mbeya Mjini), Kashaulili (Mpanda Mjini), Isanga (Mbeya Mjini), Mbalizi Road (Mbeya Mjini), Itende (Mbeya Mjini), Sinde (Mbeya Mjini), Boma (Mafinga Mjini) na Makuro (Singida Kaskazini)

Idadi hii inafanya jumla ya rufaa za wagombea Ubunge zilizofanyiwa uamuzi na Tume kufikia 117 na za wagombea Udiwani 195. Tume itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufaa hizo kila siku. Wahusika wa rufaa hizo watajulishwa kwa barua juu ya uamuzi wa Tume.


Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI